



Imefadiliwa na  
Umoja wa Ulaya



## Kuza! Kilimo cha Mazao ya Bustani kwa Maendeleo Endelevu ya Kiuchumi Zanzibar

**KUZA!** inakusudia kuimarisha mnyororo wa thamani wa kilimo cha bustani Zanzibar kwa njia endelevu ili kuongeza kipato cha kaya na kuboresha usalama wa chakula.



### TAARIFA MUHIMU

**Sekta:** Kilimo

**Mshirika Kiongozi:** Trias Tanzania

**Washirika Wengine:** Chama cha Wakulima wa Mazao ya Bustani Tanzania (TAHA), Andreas Hermes Akademie (AHA)

**Bajeti:** EUR 5 000 000

**Mchango wa EU:** EUR 4 500 000

**Muda wa Mradu:** 2020 - 2024

### USULI

Asilimia 30.04 ya wananchi wa Zanzibar wanaishi chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi na usalama wa chakula unabaki kuwa suala la mashaka makubwa. Wanawake haswa wapo katika hali ngumu kutokana na elimu ndogo na upatikanaji mdogo wa fursa za mapato na kupata nafasi chache ya kushiriki katika uongozi.

Sekta ya kilimo cha bustani inarudishwa nyuma na changamoto kadhaa kama vile ukosefu wa ujuzi na utaalamu wa sayansi ya uchumi wa kilimo na wa ujasiri amali kati ya wakulima, mbinu duni za kusimamia mazao baada ya kuvuna, ukosefu wa mikopo kwa wakulima, na uunganisho mdogo kati ya wakulima na wafanyabiashara.

Wakati huohuo, Unguja na Pemba zina uwezo mkubwa wa kuendeleza zaidi sekta ya kilimo cha bustani kutokana na maeneo hayo kuwa na udongo wenye rutuba, mvua ya kutosha na kuwa karibu na masoko ya kutumainisha. Kutumia vizuri huu uwezo ndio lengo wa mradi huu.



## AGRI-CONNECT

Kusaidia Minyororo ya Thamani kwa Ustawi wa Pamoja katika Mazao ya Kahawa, Chai na Bustani

## MAELEZO YA MRADI

- Kufunza wakulima 6,600 katika Mbinu Bora za Kilimo kwa kutumia mashamba ya kutolea mifano na Wawezeshaji wa Kijamii.
- Kufanya utafiti juu ya wadudu, magonjwa, na hasara ya mazao baada ya kuvuna.
- Kufanya utafiti wa masoko, kujenga mahusiano wa kimasoko na usambazaji wa habari za soko.
- Kutoa mafunzo ya biashara ya kilimo kwa wakulima 3,300 kwa kutumia mbinu ya AHA ya B | U | S.
- Kutoa msaada wa kibiashara kwa wafanyabiashara 50 na wasindikaji kwa kutumia mbinu ya mzunguko wa BDS ya Trias.
- Kuunda na kuimarisha vikundi vya akiba na mikopo 165 na kujenga mahusiano kati ya wahusika katika mnyororo wa thamani na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOs).
- Kushawishi na kutetea upunguzaji wa vizuizi katika sekta ya kilimo cha bustani.
- Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Viwango ya Zanzibar ili kuendeleza na kutekeleza viwango vya kilimo cha bustani.
- Kwa kushirikiana na Idara ya Usalama wa Chakula na Lishe, kukuza zana za mbegu kwa ajili ya kuanzisha bustani za jikoni, kuhamasisha kaya za wazalishaji wa kilimo cha bustani 6,600 kuhusu lishe anuwai ya lishe na mbinu zinazozingatia usafi katika utayarishaji wa chakula.
- Maendeleo wa kishirika ya TAHA: utekelezaji wa mwongozo wa Trias kuhusu maendeleo ya kijinsia; kuboresha mfumo wa habari wa dijitali wa TAHA, na kusaidia usimamizi wa mabadiliko na uongozi.

## MATOKEO YATARAJIWAYO

Mradi huu unatarajia kufikia matokeo matatu yafuatayo:

1. Minyororo ya thamani ya kilimo cha bustani ilioimariswa, yenye faida zaidi na ilio endelevu ambayo ina mashamba ya kilimo cha bustani yenye uzalishaji mkubwa zaidi, upungufu wa hasara ya mazao baada ya mavuno, na mahusiano mazuri kati ya wahusika katika mnyororo wa thamani.
2. Kuongezeka kwa lishe bora na anuwai kwa walengwa pamoja na matumizi ya mbinu zinazozingatia usafi katika utayarishaji wa chakula.
3. Kuimarishwa kwa uwezo wa Chama cha Kilimo cha Mazao ya Bustani Tanzania (TAHA) kusaidia na kuwalilisha sekta ya kilimo cha bustani nchini Tanzania.

Malengo ifikapo mwisho wa mradi (2024) ni pamoja na:

- Wastani wa mapato ya kaya kwa walengwa kuongezeka kwa angalau asilimia 25.
- Idadi ya watu walioajiriwa na wanufaikaji wa kilimo cha bustani kuongezeka kwa angalau asilimia 25.
- Kiwango cha chini cha uanuwai wa lishe kwa wanawake na watoto kuongezeka kwa angalau asilimia 25.
- Uzalishaji kwa ekari moja ya mazao lengwa kuongezeka kwa angalau asilimia 50.
- Wastani wa hasara ya mazao lengwa baada ya mavuno kupungua kwa asilimia 50.
- Asilimia 70 ya wakulima wanatumia angalau asilimia 70 ya mbinu bora za kilimo mahsus kwa mazao husika.
- Angalau watu 60,000 wanatumia mfumo wa uuzaifi wa dijitali wa TAHA.
- Angalau asilimia 50 ya wahusika katika mnyororo wa thamani wa kilimo cha bustani kupata huduma za kifedha.
- Viwango vya kilimo cha bustani vimetengenezwa na ZBS na vinafanya kazi.
- Wastani wa majibu ya utafiti kuhusu Maarifa, Mitazamo, na Tabia juu ya lishe kuongezeka kwa asilimia 25.
- Angalau asilimia 50 ya wanawake wanaolengwa ni wanachama wa TAHA.

## WASHIRIKA



ANDREAS  
HERMES  
AKADEMIE



## MAWASILIANO

### Ofisi ya TAHA Zanzibar,

Mpendae - Bin Hamran, Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 776 202 473

Barua Pepe: aziza.feruz@taha.or.tz



Imefadhilliwa na  
Umoja wa Ulaya

Email: delegation-tanzania@eeas.europa.eu

<https://www.eeas.europa.eu/delegations/tanzania>

Facebook: EuropeanUnionTanzania

Instagram: EUinTZ